

Je, ni wasiliane na niishi vipi na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI anahitaji ushauri na mara pale atakapohisi unamjali i i i i i i (unamheshimu) na kumjali, uzito wa ugonjwa unakuwa mwepesi. Mtu mwenye UKIMWI ni mgonjwa kama wagonjwa wengine, i isipokuwa anahitaji faraja zaidi kwa sababu ugonjwa wake hauna tiba. Matunzo sahihi i kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI ni muhimu, Mtu anayeishi na Virusi vya UKIMWI apate lishe bora i ili aweze kuimarisha afya yake na awe msafi wa mwili, nguo, nyumba na vyakula. Pia apatiwe matibabu haraka na kwa ukamilifu kwa maradhi yote yatakayojitokeza na asaidiwe kufanya kazi nzito. Mtu anayeishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI ana haki za binadamu kama binadamu wengine. Kumbuka kwamba rafiki au ndugu yako mwenye Virusi vya UKIMWI na UKIMWI bado ni rafiki au ndugu yako!

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25965>